



1. Je amri ya pili ni inasemaje?

\_\_\_\_\_

2. Je ni watu gani ambao Paulo aliwaandikia kuwa wamelogwa?

\_\_\_\_\_

3. Je ni mtoto gani wa Daudi aliye uliwa na Sulemani?

\_\_\_\_\_

4. Elisha alikufa kifo gani?

\_\_\_\_\_

5. Je ni nabii gani aliye simamisha mvua kwa miaka mitatu na nusu?

\_\_\_\_\_

6. Wana wa kuhani Eli wanaitwa wakina nani?

\_\_\_\_\_

7. Je Amri ya 7 inasemaje?

\_\_\_\_\_

8. Je mfalme sauli alipo weka nadhili kuwa asile mtu wawapo vitani je ni nani aliye kula akalifedhehesha jeshi?

\_\_\_\_\_

9. Je Shimei alimkosea nini Mfalme Daudi?

\_\_\_\_\_

10. Kwanini Absalomu alikamatwa mapema.

\_\_\_\_\_



## MTIHANI WA BIBLIA (part 16) (MASWALI YA BIBLIA)

Nakutakia mtihani mwema .

@NURU YA UPENDO

[www.wingulamashahidi.org](http://www.wingulamashahidi.org)

0652274252 au 0693036618

04/03/2023

MASAHIHISHO YA MTIHANI LEO

MTIHANI WA BIBLIA (part 16)

(MASWALI YA BIBLIA)

1.Je amri ya pili ni inasemaje?

Jibu. Kutoka 20:4-6

[4]Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia.

[5]Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,



[6]nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

---

2. Je ni watu gani ambao Paulo aliwaandikia kuwa wamelogwa?

Jibu. WAGALATIA

Soma. Wagalatia 3:1

---

3. Je ni mtoto gani wa Daudi aliye uliwa na Sulemani?

Jibu. ADONIA

Soma. 1wafalme 2;19-25

---

4. Elisha alikufa kifo gani?

Jibu. Alikufa kwa ugonjwa.

Soma. 2Wafalme 13;14-20

---

5. Je ni nabii gani aliye simamisha mvua kwa miaka mitatu na nusu?

Jibu. NABII ELIYA MTISHBI

Soma 1Wafalme 17;1

---

6. wana wa kuhani Eli wanaitwa wakina nani?

Jibu. Finehasi na HOFNI

Soma. 1Samweli 1;3

---

7. Je Amri ya 7 inasemaje?

Jibu. Usizini

Soma. Kutoka 20;14

---

8. Je mfalme sauli alipo weka nadhili kuwa asile mtu wawapo vitani je ni nani aliye kula



akalifedhehesha jeshi?

Jibu. YONATHANI

Soma. 1Wafalme 14;26-27

---

9.je Shimei alimkosea nini Mfalme Daudi?

Jibu. ALIMLAANI DAUDI PASIPO KOSA.

Soma. 2Samweli 16:5-14

---

10. Kwanini Absalomu alikamatwa mapema.

Jibu. Nywele zake zilikuwa ndefu sana hivyo zilinasa kwenye mti.

Soma. 2Samweli 18;9-15

---

BWANA YESU akubariki sana shea na kwa wengine pia.

@NURU YA UPENDO

[www.wingulamashahidi.org](http://www.wingulamashahidi.org)

0652274252 au 0693036618